TAARIFA YA UCHAMBUZI WA BAJETI YA KILIMO

Nafasi ya Secta ya Kilimo katika bajeti ya Serikali

"…….Msingi wa maudhui ya azma ya KILIMO KWANZA, ni kukiri kwamba, haiwezekani kukuza uchumi wa Tanzania na kiwango cha kupunguza umaskini kwa Watanzania walio wengi bila kuwekeza kwa kiwango cha kuridhisha katika Sekta ya Kilimo."

..... **Stephen Masatu Wassira,** Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; August 2010.

Taarifa hii ni matokeo ya kazi shirikishi ya uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2010/11 iliyofanywa na Mtaalam Mshauri, Bw. Marcossy Albanie, kwa niaba ya Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira (LEAT) kupitia kampeni yake ya kuendeleza sekta ya Kilimo nchini Tanzania. Mradi huu unafadhiliwa na Trust Africa.

KUHUSU LEAT

Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira (LEAT) ni taasasi ya kiraia ya kwanza ya aina yake Tanzania inayojihusisha na utetezi wa mazingira na utekelezaji wa sheria za mazingira. LEAT ilianzishwa mwaka 1994 na kusajiliwa rasmi mwaka 1995 chini ya Sheria ya Vyama vya Kiraia. Lengo lake kuu ni kuhakikisha uwepo wa mfumo na mbinu thabiti za matumizi, usimamizi na uhifadhi wa rasilimali asili na mazingira ya Tanzania.

LEAT inatekeleza tafiti za sera, Utetezi na ushawishi (Uchechemuzi) na kuendesha kesi-msingi zenye malengo ya kuinua na kuimarisha usimamizi, uelewa na matumizi bora ya mazingira na rasilimali asili za Tanzania.

Mawasiliano

Lawyers' Environmental Action Team (LEAT)
Mazingira House, Mazingira Street
Mikocheni Area
P. O. Box 12605
Dar es Salaam
Tanzania
info@leattz.org

Hali Halisi Ya Kilimo Nchini Tanzania

Awamu ya kwanza ya programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) iliyoanza 2006/07 itakamilika mwaka 2012/2013. Kupitia ASDP, Wizara inatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya kilimo ikishirikiana na Halmashauri kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Develoment Plans*- DADPs).

Mafanikio yaliyopatikana:-

i. Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini kutoka tani 241,753 mwaka 2005/2006 hadi tani 302,000 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 76. Katika kipindi hicho upatikanaji wa mbolea yenye ruzuku uliongezeka kutoka tani 53,389 hadi tani 150,000. Aidha, fedha zilizotengwa kugharamia ruzuku ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 7.48 mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 118 mwaka 2009/2010,

ii. Upatikanaji wa mbegu bora uliongezeka kutoka tani 10,477 mwaka 2005/2006 hadi tani 16,148 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 54.12.

iii. Upatikanaji wa miche bora ya mibuni uliongezeka kutoka miche milioni 2.85 mwaka 2006/2007 hadi miche milioni 10.4 mwaka 2009/2010. Aidha, upatikanaji wa miche bora ya chai uliongezeka kutoka miche milioni 2.48 hadi miche milioni 11.5 katika kipindi hicho,

iv. Kuongeza uwezo wa kutoa mafunzo kwa wataalam wa ugani katika vyuo vya kilimo nchini kutoka wataalam 650 mwaka 2005/2006 hadi wataalam 3,500 mwaka 2009/2010. Idadi ya wataalam wa ugani imeongezeka kutoka 3,379 waliokuwepo mwaka 2007/2008 hadi watalaam 4,439 mwaka 2009/2010. Aidha, katika kipindi hicho, idadi ya wakulima wa mfano wanaopatiwa mafunzo kupitia utaratibu wa shamba darasa iliongezeka kutoka wakulima 1,800 hadi wakulima 174,370 kwa kupitia mashamba darasa 6,711 na wamekuwa wakiwafundisha wakulima wenzao katika maeneo yao,

v. Kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula kutoka tani milioni 9.66 mwaka 2005/2006 hadi tani milioni 12.825 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 33. Wananchi katika maeneo yaliyokabiliwa na ukame wamekuwa wakipatiwa msaada wa chakula au kuuziwa chakula kwa bei nafuu ya shilingi 50 kwa kilo,

vi. Eneo la kilimo cha umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 264,388 mwaka 2005/2006 hadi hekta 331,490 mwaka 2009/2010 ambapo jumla ya kaya 200,000 zimenufaika na ongezeko hilo.

Ushirika:

Kati ya mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuhamasisha wananchi katika sekta mbalimbali kuanzisha au kujiunga na Vyama vya Ushirika.

Mafanikio yaliyopatikana:-

i. Idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika iliongezeka kutoka wanachama 750,000 hadi kufikia wanachama milioni 2.2 na Vyama vya Ushirika kutoka 5,730 hadi 9,501,

ii. Idadi ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) iliongezeka kutoka Vyama 1,875 hadi 5,344 sawa na ongezeko la asilimia 184.5. Idadi ya wanachama wa SACCOS iliongezeka kutoka 291,368 hadi 911,873 katika kipindi hicho sawa na ongezeko la asilimia 213,

iii. Akiba na amana za wanachama ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 85.6 hadi bilioni 194.8 sawa na ongezeko la asilimia 127.5. Mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kutoka shilingi bilioni 65.7 hadi shilingi bilioni 463.4 sawa na ongezeko la asilimia 605.3. Mikopo hiyo ilitolewa kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, biashara ndogo ndogo, ujenzi wa nyumba, elimu na matibabu.

Bajeti ya Wizara:

Bajeti ya Sekta ya Kilimo iliongezeka kutoka shilingi bilioni 233.309 mwaka 2005/2006, sawa na asilimia 5.78 ya bajeti yote ya Serikali hadi shilingi bilioni 666.9 mwaka 2009/2010 sawa na asilimia 7.8 ya bajeti yote ya Serikali.

Mchango na Ukuaji wa Sekta Ya Kilimo

Licha ya mabadiliko yaliyotokea katika mfumo wa uchumi katika miaka ya karibuni ambapo sekta za madini, utalii na huduma zimekua kwa kasi Sekta ya Kilimo inatoa mchango mkubwa katika kuwapatia ajira Watanzania zaidi ya **asilimia 70** na inachangia wastani wa **asilimia 95** ya chakula kinachohitajika nchini. Katika kipindi hicho, Sekta ya Kilimo ilikua kwa wastani wa **asilimia 4** na ilichangia **asilimia 26** ya Pato la Taifa.

Malengo ya Kilimo Kimataifa

Kulingana na mpango wa kimataifa wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia, lengo namba moja (MDG1): Kufuta umasikini uliopindukia na njaa, unayo malengo madogo matatu:

i. **Lengo dogo 1(a):** kupunguza kwa nusu ya kiwango cha watu wanaoishi kwa kutegemea dollar moja kwa siku,

ii. **Lengo dogo 1(b):** kuhakikisha upatikanaji wenye kuaminika wa kazi halali kwa wote ikiwemo akinamama na vijana,

iii. **Lengo dogo 1(c):** kupunguza kwa nusu ya kiwango idadi ya watu wanaoteseka kwa njaa.

MAMBO YA MSINGI JUU YA UMASIKINI TANZANIA



Taarifa ya Ufafanuzi kutoka kwenye Jedwali

- Umasikini kwa Tanzania ni suala lenye uhusiano wa karibu na maisha ya vijijini ambako ndiko watu wengi masikini wanaishi.
- Maeneo ya vijijini Tanzania ndiko kwenye miundombinu mibovu ya kiuchumi na kijamii kiasi cha kuathiri maisha ya jamii iishiyo huko. Hali hii mbaya inajumuisha miundombinu ya Elimu, Afya, Maji, Barabara, Umeme na hata huduma za kijamii na ugani.
- Asilimia zaidi ya 74 ya masikini huishi vijijini wakitegemea kilimo.
- Zaidi ya 37% ya wakazi wa vijijini huishi chini ya kiwango cha umasikini, 24% huishi maeneo ya mijini na 16% tu ya wakazi wa Dar es salaam ndio masikini hivi.
- Zaidi ya 80% ya uzalishaji mazao ya chakula hufanywa na wazalishaji wadogo vijijini wenye mashamba kati ya nusu eka na eka moja tu. Zaidi ya 60% ya wazalishaji hawa wadogo ni wanawake.

- Kilimo huchangia 26% ya pato la Taifa ingawa hupata bajeti ya chini ya 7% na ambayo kiwango chake huathiriwa zaidi kwa ajili ya mdororo wa thamani ya shilingi.

- Mchango wa sekta ya kilimo kwenye pato la Taifa (GDP) linapungua huku ukuaji wa sekta wenyewe ukibaki bila tija na kukwama. Hii haijalishi hoja kuwa ziko changamoto kadhaa katika sekta ya kilimo ambazo hazijafanyiwa kazi kabisa.

Mwelekeo wa Bajeti na Matumizi ya Wizara ya Kilimo

Mwaka wa fedha	Jumla ya Bajeti ya Kilimo (Bilioni)	Jumla ya Bajeti ya Taifa (Bilioni)	Ukuaji wa Bajeti ya Kilimo kwa Asilimia (%)	Asilimia ya Bajeti ya Kilimo kwenye Bajeti ya Taifa.	Mabadiliko ya asilimia katika Mgawanyo wa Bajeti ya kilimo
2001/02	52.1	1,764.7		3.0	
2002/03	84.5	2,219.2	62.2	3.8	0.8
2003/04	148.6	2,607.2	75.9	5.7	1.9
2004/05	157.7	3,347.5	6.1	4.7	-1.0
2005/06	233.3	4,035.1	48.0	5.8	1.1
2006/07	276.6	4,788.5	18.5	5.8	0.0
2007/08	372.4	6,000.0	34.6	6.2	0.4
2008/09	440.1	7,216.1	18.2	6.1	-0.1
2009/10	666.9	9,500.0	34.0	7.0	0.9
2010/11	903.8	11,610.0	26.2	7.8	0.8
2011/12	926.0	13,500.0	2.7	6.9	-0.9

Pamoja na kuongezeka kwa bajeti ya wizara, kumekuwa na kupungua kwa matumizi ya ***uendeshaji shughuli za ofisi*** *kwa kasi huku kiwango cha matumizi kwa* ***shughuli za maendeleo*** *yakiongezeka. Hata hivyo kiwango cha matumizi kwenye shughuli za maendeleo ya kilimo ikilinganishwa na matumizi kwenye shughuli za uendeshaji wizara na idara za kilimo bado kipo* ***chini ya matarajio (50/50).***

Hata hivyo miongoni mwa matumizi yaliyoongezeka kwa wizara ni pamoja na matumizi ya maendeleo ya mazao na upatikanaji pembejeo na zana za kilimo. Pamoja na matumizi na vifungu vya matumizi kubadilika na kutokuwa rahisi kufuatilika, mwelekeo wa matumizi ya Wizara yanaonekana kulenga zaidi kuimarisha maendeleo ya mazao ya chakula na biashara. Mgawanyo huu unamaanisha kuwa huenda umuhimu ulowekwa kwa wizara kuongezewa bajeti umetokana na mahitaji ya taifa kujitosheleza kwa chakula na au ni matokeo ya mfululizo wa upungufu wa chakula Tanzania uloshuhudiwa katika miaka ya 2006 – 2010.

MWELEKEO WA MATUMIZI	2007/08	2008/09	2009/10
Utawala na Uendeshaji	2,836,147,400	1,783,424,200	2,703,556,000
ofisi ya fedha	547,317,000	828,702,800	1,111,642,000
Sera na Mipango	1,166,243,600	1,435,774,100	1,428,776,600
Vyuo vya Mafunzo Kilimo	2,029,599,000	1,161,330,500	6,176,259,000
ukaguzi wa Ndani	0	100,000,000	249,117,000
Ugavi/Ununuzi	0	340,000,000	443,278,000
Elimu, Habari na Mawasiliano	0	350,000,000	394,217,000
Kitengo cha TEHAMA	0	200,000,000	247,235,000
sheria	0	0	286,683,000
Usimamizi Mazingira	0	0	216,548,000
Maendeleo ya Mazao	35,842,155,400	88,927,377,900	81,004,015,100
Zana za Kilimo	2,200,466,000	1,612,712,500	689,326,000
Matumizi Bora Ardhi	0	400,000,000	462,329,000
Uzalishi Mbegu	0	160,000,000	232,015,100
Utafiti kilimo	13,377,357,100	14,142,914,200	13,927,709,200
Maendeleo Ushirika	6,332,474,700	5,292,876,700	5,811,790,100
Usalama Chakula	867,622,800	16,969,105,100	20,485,837,000
Hifadhi ya Nafaka	5,638,000,000	0	0

Matumizi katika Pembejeo na Mbolea

Msimu	Mbolea(000 tons)	Mbegu Bora (000 tons)	Mgao (Billion TSh)	Kiwango % ya Bajeti ya Kilimo
2003/04	39.4		2.0	1.3
2004/05	81.8		7.2	4.6
2005/06	63.0		7.5	3.2
2006/07	89.9	0.8	21.0	7.6
2007/08	83.0	1.1	19.5	5.2
2008/09	155.0	6.0	71.5	16.2
2009/10	150.0	15.2	102.8	15.4
2010/11	200.0	20.0	146.0	16.2

Takwimu za wizara zinaonesha kuongezeka kwa kasi sana kiasi kinachotengwa na hata kinachotumika kwenye manunuzi na usambazaji mbolea kwa wakulima kwa mfumo wa mbolea ya ruzuku kutoka Tshs. 2.0 bilioni hadi Tshs. 146 bilioni huku kiwango cha mbolea na mbegu za ruzuku vikiongezeka kutoka tani 39,400 hadi 200,000 na 0 hadi 20,000 kwa kipindi cha 2003/04 hadi 2010/11.

Uwekezaji katika Umwagiliaji

Kumekuwepo na ongezeko kubwa la bajeti ya uwekezaji katika miradi ya umwagiliaji kuanzia mwaka 2006/07 serikali ilipoanza kutilia mkazo kilimo cha umwagiliaji maji. Miradi ya umwagiliaji maji vijijini imeongezewa bajeti kupitia halmashauri toka 200 milioni hadi 4.6 bilioni mwaka 2008/09. Hata hivyo kwa mwaka 2007/08 serikali ilitenga 7.4 bilioni kwa miradi ya maji kupitia halmshauri. Bajeti hii pia imeongezeka toka bilioni 1.3 hadi 3.4 kwa mwaka 2006/07 hadi 2008/09.

Kielelezo cha Uwekezaji katika Umwagiliaji

Eneo	2006/07	2007/08	2008/09
Mfuko wa Maendeleo wa Umwagiliaji wa Wilaya (DIDF)	0.2	7.4	4.6
Mfuko wa Maendeleo wa Umwagiliaji wa Taifa (NIDF)	1.3	3.2	3.4
Total	**1.5**	**10.6**	**8.0**

Bajeti ya Mwaka 2011/12

Mwaka 2011/2012 wa fedha ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Serikali, 2011 – 15 wenye nguzo kuu zifuatazo:-

- Kuimarisha ukuaji wa Uchumi na kuhakikisha mafanikio yaliyokwisha patikana yanaimarisha huduma za jamii
- Kutumia rasilimali zilizopo kuwa kichocheo cha maendeleo jumuishi.
- Kuhakikisha nchi inafaidika kwa nafasi yake ya kijiografia,
- Kuinua matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Kwa kuzingatia haya, bajeti ya mwaka 2011/12 imelenga kutanzua changamoto zifuatazo:-

- Gharama kubwa ya maisha na ukosefu wa ajira kwa vijana,
- Kuinua mapato ya ndani ya serikali kwa kuongeza uwekezaji wa serikali kwenye maeneo yanayosisimua uchumi na kutanua vyanzo vya mapato

Kwa kuzingatia malengo haya, serikali imegawanya bajeti yake kwa vipaumbele: Maji, Uchukuzi na Miundo-mbinu ya Usafirishaji, Kilimo na Umwagiliaji, na kuongeza ajira kwenye sekta binafsi na sekta za umma.

Mgawanyo wa Bajeti kisekta kwa mwaka wa Fedha 2011/12.



Angalizo: *Ni muhimu kutambua kuwa mgawo wa sekta ya kilimo hauonekani vema iwapo tukiangalia mgao wa bajeti kwa wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pekee. Hii inatokana na mgawanyo wa majukumu kiwizara ambapo kuna wizara nyingine tofauti na wizara husika ambazo Bajeti zake zinalenga masuala mbalimbali yanayohusiana na sekta ya Kilimo.*

Mfumo wa bajeti na uendeshaji serikali Tanzania unagawanya matumizi ya usimamizi na maendeleo ya kilimo katika wizara tano za kisekta; OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Wizara mama ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwa ujumla huu, wizara hizi zimetengewa jumla ya Tshs.639.7 bilioni ambapo takribani Tshs. 307.5 bilioni zimeelekezwa moja kwa moja katika kuendeleza kilimo.

Kielelezo:


Mapato ya Nje/Misaada, 869.4 bn
Mapato ya Ndani/Kodi, 7,126.4 bn
Mikopo/Ruzuku, 5,530 bn
BAJETI KUU 2011/12
TZS 13,526 BILION


BajetiKuu, 13,526 bn
Uendeshaji, 3,419.6 bn
Mishahara 3,270 bn
Deni la Taifa, 1,910 bn
Maendeleo 4,925 bn
Uendeshaji Kilimo
Mishahara Kilimo
Maendeleo Kilimo 307.5 bn
KCU 249.45 bn
MAJI 9.13bn
MIFUGO 6.73bn
TAMISEMI 41.71bn
UJENZI 0.48bn



Mgawanyo wa Fedha za Maendeleo ya Kilimo, Chakula na Ushirika:

Mgawanyo huu unatuonesha namna ambavyo serikali imejikita kutatua matatizo ya upatikanaji wa chakula kwa kuimarisha huduma za maendeleo ya mazao na usalama wa chakula. Hata hivyo inaonekana kushindwa kuwekeza vya kutosha katika Nyanja muhimu za kuimarisha miundombinu.

Utekelezaji Bajeti na Ufanisi

Kwa mujibu wa taarifa zilizopo za hadi ya tarehe 31 Machi 2011, matumizi ya fedha zilizogawiwa kwenye Sekretarieti za mikoa ni shilingi 1,202 milioni, OWM-TAMISEMI ni 204,250 milioni na 23,300 milioni kwa Serikali za Mitaa ambazo pia ilishaingiza kwenye mikataba shilingi 16,980 milioni kwa shughuli mbalimbali. Hii ni asilimia 66 kwa mikoa, 78% TAMISEMI, 34% kwa zilizotumika Halmashauri na 25% ya fedha zilizotolewa ndizo zilizoingizwa kwenye mikataba. Juu ya matumizi haya, Halmashauri nchini zilitumia shilingi 33.18 bilioni ya ruzuku za ASDP na 3.18 bilioni kutoka

vyanzo vingine zilizokuwa zimebaki mwaka 2009/10.

Kwa ujumla utekelezaji na ufanisi wa matumizi umeonekana kuwa wenye kiwango kinachokubalika kwa kuzingatia viwango vya matumizi, yaani 59%, 65% na 78% kwa Halmashauri, Sekretarieti za Mikoa na TAMISEMI.

Vipaumbele vya matumizi

Pamoja na kuwa bajeti ya kilimo, chakula na ushirika (KCU) iliainisha wazi vipaumbele vyake:

1. Miundombinu ya uzalishaji na masoko ya kilimo na mifugo,
2. Kuongeza na kuboresha matumizi ya zana za kilimo na mifugo,
3. Kutanua na kuimarisha miundombinu ya afya za mifugo,
4. Kutoa huduma bora za ugani,
5. Kuinua kiwango cha ufahamu na matumizi ya utaalamu wa kilimo kwa wakulima, na
6. Kushughulikia maswala mtambuka katika kilimo na mifugo ikiwemo utawala bora na kupambana na UKIMWI/VVU.

Hata hivyo matumizi halisi (kushoto) yanaonekana kutoa picha tofauti. Hakuna uhakika hata kidogo kuwa matumizi haya yanaweza kutimiza malengo yaliyotarajiwa ikizingatiwa kuwa imebaki miezi mitatu tu kukamilika mwaka wa fedha wa 2010/11.

Pamoja na bajeti hizi katika wizara zote za kisekta zinazochangia maendeleo ya kilimo, maboresho ya sheria na mfumo pia yamefanyika ili kuweka mazingira mazuri kuwezesha kukua kwa sekta hii:-

1. Mabadiriko katika sheria ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kutoa nafuu na misamaha ya kodi kwa mitambo na vipuri vya mashine za kuvunia mazao, kukaushia na kukoboa mpunga, matrekta ya kupandia, matela, matrekta madogo (Powertillers) na mashine zingine za mashambani na kilimo.
2. Kufutwa kwa baadhi ya kodi za usafirishaji nje samaki na hivyo kuwezesha wauza samaki nje kuongeza biashara na mauzo.

Changamoto

Taarifa hizi zinaainisha changamoto kadhaa katika utekelezaji mipango na bajeti za serikali kwa sekta za kilimo, mifugo na ushirika:

1. Bajeti ya kilimo imeonekana kuendelea kuwa chini ya kiwango kilichokubaliana kimataifa kupitia Tamko la Maputo la mwaka 2003 na Programu Kabambe ya Kuendeleza Kilimo Afrika (CAADP) ambavyo vinazitaka nchi zilizosaini, Tanzania ikiwemo, Kuongeza Bajeti ya sekta ya Kilimo kufikia angalau asilimia 10 ya Bajeti ya jumla ifikapo 2010. Hii inaonekana hata miaka 7 baada ya Tanzania kuridhia CAADP. Kiwango cha bajeti kimeendelea kuwa 6.9%.

2. Kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo imeendelea kuwa chini ya matarajio ya CAADP ya 6% ambapo hadi 2010/11 kimeendelea kuwa 4.3% au chini yake.

3. Bajeti imeshindwa kuzingatia mdororo wa thamani ya shilingi na hivyo kupunguza uwezo wa wizara na idara zake kutumia bajeti kutekeleza matakwa na malengo yaliyokusudiwa. Ikilinganishwa na mwaka 2009/10 bajeti ya 2010/11 ni pungufu kwa bilioni 11.

4. Taarifa zinabainisha uwezo mdogo wa kitaalam wa watendaji ngazi za mikoa kwa ajili ya kusaidia utendaji ngazi za Halmashauri (Hata hivyo taarifa zisizo rasmi zinaaonesha kuwa watendaji wa kilimo na mifugo nchini ndio wenye mafunzo ya hali za juu kabisa wakijumuisha PhD na digrii zingine za juu).

5. Kuchelewa kwa fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri: inaonekana kuwa fedha nyingi kwa mwaka hupelekwa Halmashauri na Taasisi zingine za utendaji kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha, yaani kati ya Januari na Machi.

6. Kukosekana au kupelekwa kwa Matrekta yasiyofaa kwenye baadhi ya maeneo; mpango wa Kilimo Kwanza na uamuzi wa kusambaza matrekta madogo ya 'PowerTiller' umeonekana kutozingatia mahitaji halisi ya kila maeneo ya kilimo. Kuna wilaya na hata tarafa zenye mahitaji maalum ya matrekta na vifaa vinginevyo kuzingatia hali ya udongo, hali ya hewa na au aina ya kilimo kinachofanyika.

7. Kutokuwepo wataalam wa kutosha wenye fani na ujuzi wa kusimamia miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

8. Cha kushangaza sana ni pale ambapo rushwa na ufisadi haviguswi katika taarifa hizi za utekelezaji mipango na bajeti za sekta.

Mapendekezo

1. Kuweka na mfumo wa ufatiliaji wa fedha zilizopangwa kwa ajiri ya kilimo katika wizara nyingine ili kuhakikisha zinatimiza malengo yaliyokusudiwa na serikali.

2. Vipaumbele vilivyohainishwa na wananchi viwezwe kuzingatiwa na si kubadilisha vipaumbele kwa mujibu wa wananchi kama ilivyo sasa.

3. Kuwepo na ufatiliaji wa miradi inayotekelezwa kutoka serikalini ili kuhakikisha kuwa imefanyiwa kazi na kama imefanyiwa kazi iwe imefanyika kiukamilifu.

4. Kuwepo na sehemu ya kupata taarifa kuhusu bajeti na pia madiwani wapewe muda wa kupitia bajeti ili waweze kuchangia kiukamilifu vipaumbele vya wananchi.

5. Miradi inayofanywa na taasisi binafsi itofautishwe na ile inayofanywa na serikali ili kuondoa udanganyifu mkubwa unaofanywa na baadhi ya viongozi wa serikali.

Hitimisho

Kulingana na yale yote yaliyojadiliwa katika dondoo hili, ni dahili kwamba kazi kubwa bado inaitajika katika kukuza secta ya kilimo nchini Tanzania. Ni jukumu la viongozi wa serikali kuanzia ngazi za chini kabisa kufatilia mchakato mzima wa bajeti na kuhakikisha mchango wao katika hiyo bajeti unapelekwa bungeni kupitishwa. Bajeti ni fedha za wananchi na lazima waone matunda ya fedha zao. Kwahiyo kuna umuhimu mkumbwa kwa viongozi wa wananchi kuanzia ngazi ya chini mpaka juu kufuatilia kwa ukaribu mchakato mzima wa bajeti na kuzingatia vipaumbele vilivyo ainishwa katika maeneo yao vinafanyiwa kazi. Hivyo basi, secta ya kilimo ambayo ni uti wa mgongo wa taifa letu Tanzania kutengewa kiasi kikubwa cha bajeti ili kuinua uchumi wa nchi pia kuinua wananchi kiuchumi na kujikwamua katika umasikini.

TRUSTAFRICA